

**OFISI YA RAIS
TAWALA ZA MIKOZA NA SERIKALI ZA MITAA
HALMASHAURI YA WILAYA LIWALE**



**-0713943756 - MKUU
-00629376019- MAKAMU 1
-0686142921- MTAALUMA MWANDAMIZI**

**JINA.....
SLP 139
LIWALE.**

**SHULE YA SEKONDARI LIWALE,
S.L.P. 139,
LIWALE
14/12/2020**

**YAH: MAAGIZO YA KUJIUNGA KIDATO CHA KWANZA SHULE YA SEKONDARI
LIWALE DAY MWAKA 2021.**

1. Utangulizi

Rejea kichwa cha habari hapo juu.

Nafurahi kukujulisha kuwa umechaguliwa kujiunga kidato cha kwanza mwaka 2020 katika shule ya sekondari **LIWALE**. Shule itafunguliwa tarehe 11/01/2021 wewe unatakiwa kulipoti hapa shulenii tarehe 11/01/2021 bila kukosa. Shule ya sekondari **LIWALE** ipo magharibi mwa makao makuu ya Wilaya barabara iendayo Makata **KM 2** toka Boma la zamani.

2. Mambo muhimu ya kuzingatia:-

▪ SARE ZA SHULE:-

WASICHANA:-

- (i) Sketi za rangi ya kijani . **Sketi ivuke magoti na ifike katika vifundo vya miguu**
- (ii) Mshono wa sketi uwe wa **RINDA BOKSI**
- (iii) Mashati 2 meupe , mikono mifupi , kitambaa cha tetroni
- (iv) Viatu vyeusi, vya ngozi, vya kutumbukiza, vya kufunga kwa kamba au gidamu na visiwe vya kupanda au vya gorofa au vyenye kisigino.
- (v) Soksi nyeupe jozi/pea 2 au zaidi
- (vi) Tai rangi ya kijani sawa na ile ya kitambaa cha sketi
- (vii) **HIJABU** inaruhusiwa siyo lazima. Kama utaamua kuwa na **HIJABU** iwe nyeupe **ISIYOVUTIKA** ambayo itavaliwa na sare ya shule na light bluu ambayo itavyaliwa siku au wakati wa kazi za nje. **MITANDIO HAIRUHUSIWI**

➤ **MSHONO WA HIJABU** – Nusu kanzu mikono mirefu

WAVULANA:-

- (i) Suruali 2 za rangi ya khaki upana wa suruali chini usipungue inchi 16
- (ii) Mashati 2 meupe mikono mifupi , kitambaa cha tetroni
- (iii) Soksi nyeusi jozi/ pea 2 au zaidi

- (iv) Viatu vyeusi, vya ngozi, vya kutumbukiza, vya kufunga kwa kamba au gidamu, na visiwe vya kupanda au vya gorofa au vyenye kisigino.
- (v) Tai rangi ya khaki sawa na ile ya kitambaa cha suruali
- (vi) Mkanda mweusi wa ngozi usio na picha , urembo wala maandishi

MSISITIZO:-

1.Wazazi na wanafunzi wanapaswa kuzingatia maelekezo yaliyotolewa kuhusu sare. Wakati mwingine wanafunzi kwa matakwa yao binafsi humwamuru fundi kushona sketi fupi au suruali iliyobana na iliyochongolewa. Mavazi ya aina hiyo hayatakubaliwa. **EPUKA USUMBUFU NA KERO MAPEMA. ZINGATIA MAELEKEZO ULIYOPWEWA**

2. MWANAFUNZI YEYOTE ATAKAYEHARIBU MALI /SAMANI YOYOTE YA SHULE, MZAZI WAKE ATAWAJIBIKA KUILIPA.

UVAAJI WASARE:-

STAILI ZIFUATAZO ZA UVAAJI WA SARE YA SHULE HAZITARUHUSIWA:-

- (i) Kushusha au kulegeza suruali /kuvaan mlegezo
- (ii) Kuvaan sare ya shule bila kuchomekea shati
- (iii) Kwa wavulina kuvaan sare bila kuchomekea shati na kufunga mkanda
- (iv) Kwa wasicha kuvaan sketi fupi au isiyovuka magoti ni kosa
- (v) Kuvaan viatu bila siksi ni kosa
- (vi) Kuvaan sare bila tai hairuhuswi

▪ Nguo za michezo:-

- (i) Bukta rangi yoyote na fulana za njano kwa wavulana
- (ii) Truck –suit za rangi ya bluu kwa wasichana
- (iii) Viatu aina ya raba kwa wote

▪ Vifaa vya darasani:-

- (i) Madaftari makubwa /kaunta yasiyopungua kumi
- (ii) Biki/peni/kalamu
- (iii) Mkebe wa hesabu

3. SHERIA ZA SHULE :-

A. HESHIMA KWA UJUMLA :-

- (i) Kila mwanafunzi lazima asimame na kuamkia kwa mwalimu au mtu yeyote aliyemzidi umri.
- (ii) Ni kosa kwa mwanafunzi kutumia lugha chafu ya matusi , kashifa au kejeli
- (iii) Unatakiwa kukimbia unapoitwa au kutumwa na mwalimu au mtu yeyote
- (iv) Unatakiwa kuheshimu bendera ya taifa, wimbo wa taifa, picha za viongozi wa serikali nembo ya taifa nk.
- (v) Mwanafunzi lazima anyoshe mkono na kusimama anapouliza au kijibu swalii
- (vi) Mwanafunzi haruhuswi kupiga kelele darasani na ni kosa kutoka darasani bila ruhusa ya mwalimu au kiongozi wa darasa

(vii) Mwanafunzi haruhuswi:-

- Kuvuta sigara
- Kugombana
- Kuvaan mavazi yasiyo naheshima, kuvaan pete, heleni, bangili , mkufu nk.
- Kufuga ndevu , nywele ndefu , kucha

- Kufanya biashara akiwa shulenii
- Kupaka wanja , dawa ya kucha , dawa ya nywele na kujichbua
- (viii) Heshima kwa viongozi, wazazi , wanafunzi wote , wanafunzi wengine na jamii kwa ujumla
- (ix) Unatakiwa kuhudhuria katika kila shughuli ya shule kadri itakavyopangwa
- (x) Kutunza usafi wa mwili , mavazi na mazingira ya shule
- (xi) Kuvalaa sare ya shule wakati wote unapotakiwa
- (xii) Kuzingatia ratiba ya shule wakati wote
- (xiii) Kutunza mali ya umma

B. SHERIA ZA KWENYE MAZINGIRA YA SHULE:-

- Hairuhusiwi mwanafunzi wa kiume kuingia vyoo vya kike na mwanafunzi wa kike kuingia vyoo vya kiume
- Mwanafunzi haruhusiwi kuendesha mukutano bila kibali cha mkuu wa shule
- Mwanafunzi ni lazima atumie lugha ya kiingereza awapo shuleni isipokuwa wakati wa somo la Kiswahili mgeni yeoyote wa mwanafunzi ni lazima aripoti kwanza kwa mwalimu wa zamu
- Mwanafunzi wa utwa haruhusiwi kwenda mabwenini isipokua kwa ruhusa maalumu.

C. MWANAFUNZI HARUHUSIWI KUTEMBELEA AU KUINGIA SEHEMU ZIFUATAZO:-

- Chumba /vyumba cha/vya mwalimu/waalimu
- Nyumba ya mwalimu
- vilabu vya pombe
- Majumba ya starehe
- Nyumba za kulala wageni (**Guest House**)

D. KUFUKUZWA SHULE :-

Makosa yafuatayo yanasaababisha mwanafunzi kufukuzwa shule:-

- (1) Wizi
- (2) Ubakaji/ushoga
- (3) Utoro wa muda mrefu
- (4) Makosa ya jinai
- (5) Ulevi na matumizi ya dawa za kulevyia ikiwemo bangi na nyinginezo
- (6) Kuharibu kwa makusudi kwa mali ya umma
- (7) Kupigana au kupiga mwenzako
- (8) Kudharahu bendera ya taifa kuolewa au kuoa
- (9) Kupata mimba au kusababisha mimba ndani au nje ya shule
- (10) Kutoa mimba
- (11) Kugoma kuchochea na kuongoza au kuvuruga amani na usalama shuleni.
- (12) Kukataa adhabu iliyotolewa na mwalimu au kiongo]zi
- (13) Kujificha polini kwa lengo la kutoroka vipindi au shule kwa ujumla
- (14) Kuwa na simu ya mkononi

.....
**MWENDA, M O
MKUU WA SHULE**

VIAMBATANISHO

1. Fomu ya vipimo Hospitali (**Medical Examination Form**)
2. Fomu ya maelezo binafsi ya mwanafunzi
3. Fomu ya mzazi kukiri maelekezo

FORM 1.

MEDICAL EXAMINATION

LIWALE SECONDARY SCHOOL
P.O.BOX 139
LIWALE
14/12/2021

TO THE MEDICAL OFFICER
ANY. GOVERNMENT HOSPITAL

Ref. _____ **(Name in full)**

Please may you examine the above named as to his/her physical and mental fitness/unfitness to undertake secondary school studies and other school activities in general.

- I. Eyesight
- II. Hearing.....
- III. T.B Test.....
- IV. Pregnancy (**for girls**).....
- V. Any other serious cases.....

MEDICAL CERTIFICATION (To be completed by a government medical officer)

I have examined the above named and consider that she/he is physically and fit/unfit for full time student

- I. Eyesight
- II. Hearing.....
- III. T.B Test.....
- IV. Pregnancy.....
- V. Others.....

Name of medical officer _____ **signature** _____

Date _____

Official Stamp .

FORM 2.MAELEZO BINAFSI YA MWANAFUNZI

1. **Mimi**(mwanafunzi)-----nakubali/sikubali nafasi hii ya kujiunga na elimu ya sekondari katika shule ya sekondari **LIWALE**.
2. Naahidi kuwa ,wakati wote wa uwanafunzi wangu hapa shulenii nitakuwa mtiifu na nitafuuta sheria za shule kama zilivyoelekezwa.
3. Naahidi kuwa sitashiriki katika migomo ya aina yoyote ile hapa shulenii,wala fujo za aina yoyote,wala kutenda makosa yoyote ya jinai.
4. Naahidi pia sitakuwa mtoro wa shule wala vipindi vya darasani
5. Saini ya mwanafunzi-----tarehe-----

3.FORM 3.MAELEZO YA MZAZI

- 1.Mimi -----mzazi wa mwanafunzi-----
- 2.Nakubali/sikubali nafasi aliyopewa motto wangu ambaye ni-----
- 3.Nakiri/Sikiri na nakubali/Sikubali sheria na maelekezo yote yaliyotolewa na shule.

4.Saini ya mzazi-----

5.Tarehe.....